



TAARIFA KWA UMMA

HUDUMA ZA KUBADILISHA FEDHA ZA KIGENI

Mnamo mwezi Novemba mwaka 2018, Benki Kuu ya Tanzania iliratibu operesheni maalum ya maduka ya kubadilisha fedha za kigeni na baadhi ya maduka bubu ambayo hayana leseni lakini yalikuwa yakiendesha biashara hiyo kinyume na sheria katika mkoa wa Arusha. Kutokana na operesheni hiyo, maduka hayo yalifungwa kwa muda kupisha uchunguzi unaoendelea kwa lengo la kubaini maduka yaliyokuwa yanaendesha biashara kinyume na sheria, ikiwemo kutumika katika biashara haramu ya utakasishaji fedha, ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa.

Benki Kuu inapenda kuutaarifu umma kuwa huduma za kubadilisha fedha za kigeni kwa sasa zinapatikana katika mabanki na taasisi za fedha zinazoendesha biashara nchi nzima. Aidha, Benki Kuu imeyahimiza mabanki na taasisi za fedha kuendelea kutoa huduma za kubadilisha fedha za kigeni kwa wateja wote, wakati uchunguzi wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni na maduka bubu unaendelea. Wananchi watakaopata usumbufu wowote wanaombwa kutoa taarifa Benki Kuu kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

Benki Kuu pia inapenda kuutahadharisha umma kutotumia huduma zisizo rasmi za ubadilishaji wa fedha za kigeni kutokana na hatari mbalimbali zinazotokana na huduma hizo, ikiwemo kuibiwa au kupewa fedha bandia. Aidha, utumiaji wa huduma zisizo rasmi ni kinyume na sheria za nchi. Hatua kali zitachukuliwa dhidi ya watoaji na watumiaji wa huduma hizo (*black-market*).

BENKI KUU YA TANZANIA

JANUARI 31, 2019